

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:
Simu: 2203156/2203158
Fax: +25522203213
Tovuti: www.dsm.go.tz
Barua pepe : ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA,
3, Barabara ya Rashid Kawawa,
S.L.P. 5429,
12880, DAR ES SALAAM.
Tanzania

22 Agosti, 2020

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

MKUU WA MKOA WA DAR ES SALAAM AKUTANA NA WALIMU, AWAHAKIKISHIA KUWA SERIKALI ITAENDELEA KULIPA MALIMBIKIZO YOTE WANAYODAI.

Mkuu Wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Abubakar Kunenge leo amefanya kikao kazi na mamia ya walimu wa Shule za Msingi zilizopo Wilaya ya Ilala kwa lengo la kujadili changamoto zinazowakabili na kuangalia namna bora ya kuendelea kuboresha hali ya elimu ambapo amewahakikishia Walimu kuwa Serikali inaendelea kulipa malimbikizo yote wanayodai.

RC Kunenge amesema hayo baada ya Kikao na walimu wa Ilala pia amepanga kukutana na Walimu Wa Wilaya nyingine za Mkoa huo ili aweze kuzipatia majibu changamoto zinazowakabili ambapo amewapongeza walimu wote Wa Mkoa huo kwa kazi nzuri wanayoifanya jambo linalofanya Mkoa huo kuwa kinara wa ufaulu kila mara.

Aidha Mkuu huyo wa Mkoa amemuelekeza Mkurugenzi Wa Manispaa ya Ilala kuhakikisha anatoa kipaumbele cha ajira kwa walimu ili kuweza kukidhi changamoto ya uhaba Wa walimu Kwa baadhi ya shule.

Pamoja na hayo Mhe. Kunenge amekemea vikali vitendo vya kuvuja Kwa mithihani kwa baadhi ya shule za sekondari na kuwataka wahusika kuwa makini na jambo hilo ili lisiweze kuchafua sifa nzuri ya Mkoa. Hata hivyo RC Kunenge ametoa wito Kwa Walimu na wananchi Wa mkoa huo kuhudhuria mikutano ya Kampeni za wagombea mbalimbali ili waweze kuchagua viongozi wenye kuleta maendeleo.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano
OFISI YA MKUU WA MKOA
DAR ES SALAAM